BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2018

## 614 MAARIFA YA JAMII

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA A GATCE 2018

# 614 MAARIFA YA JAMII

*Kimechapishwa na:*

Baraza la Mithani la Tanzania,
P.O. Box 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mithani la Tanzania, 2018**

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO


DIBAJI .................................................... iv

1.0 UTANGULIZI .................................................... 1

2.0 TATHMINI YA MAJIBU YA MTAHINIWA KWA KILA SWALI .................... 2

2.1 SEHEMU A: TAALUMA .................................................... 2

2.1.1 Swali 1. Sayari Dunia .................................................... 2

2.1.2 Swali 2. Nchi yetu Tanzania .................................................... 4

2.1.3 Swali 3: Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani .................................... 7

2.1.4 Swali 4. Nchi Yetu Tanzania .................................................... 9

2.1.5 Swali 5. Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani .................................... 12

2.1.6 Swali 6. Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika .................................................... 15

2.1.7 Swali 7. Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika .................................... 18

2.1.8 Swali 8. Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi katika Afrika Huru .................................................... 20

2.1.9 Swali 9. Ushirikiano wa Kimataifa .................................................... 22

2.1.10 Swali 10. Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika Huru ………………………………………………………….. ....... 24

2.2 SEHEMU B: TAALUMA .................................................... 27

2.2.1 Swali 11. Sayari Dunia .................................................... 27

2.2.2 Swali 12. Nchi Yetu Tanzania .................................................... 33

2.2.3 Swali 13. Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika .................................................... 38

2.2.4 Swali 14. Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika .................................... 43

2.3 SEHEMU C: UFUNDISHAJI .................................................... 49

2.3.1 Swali 15. Maandalizi ya Kufundisha na Kujifunza .................................... 49

2.3.2 Swali 16. Uchambuzi wa Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia .............. 52

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA ........... 56

4.0 HITIMISHO .................................................... 59

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO .................................................... 59

KIAMBATISHO .................................................... 61

## DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa wa Mtihani wa Maarifa ya Jamii, Ualimu Daraja A ngazi ya cheti, imetayarishwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, wakufunzi, watunga sera pamoja na wadau wengine wa elimu. Mitihani ni sehemu mojawapo muhimu ya mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ambayo huwezesha kutoa tathmini ya namna utekelezaji wa mtaala wa ngazi husika ulivyofanyika. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa Maarifa ya Jamii ngazi ya cheti utawezesha kutoa mrejesho kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Jiografia na Historia. Majibu ya watahiniwa katika mtihani huweza kuashiria viwango na ubora wa mielekeo, stadi na maarifa ambayo watahiniwa wameweza kuyapata katika kujifunza taaluma na utalaam wa kufundisha katika miaka miwili ambayo wanachuo wamekuwa katika mafunzo.

Katika kufanya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa, sababu zilizofanya watahiniwa kujibu maswali vizuri au kushindwa kujibu maswali vizuri zimeainishwa. Uchambuzi wa kila mada na kiwango cha kufaulu katika mada husika pia umefanyika na sababu za mada hizo kufanyika vizuri au vibaya kubanishwa.

Uchambuzi wa majibu uliofanyika unaonesha kuwa, watahiniwa walio wengi walifaulu Mtihani wa Maarifa ya Jamii kwa kiwango kizuri. Aidha, uchambuzi umeonesha kuwa, watahiniwa wengi waliofanya mtihani wa Maarifa ya Jamii waliweza kuelewa matakwa ya maswali ya mtihani huo, na hivyo kuwawezesha kutoa majibu yaliyokidhi mahitaji ya maswali hayo. Watahiniwa walionesha kuwa na maarifa, stadi na mielekeo waliyotarajiwa kuwa nayo ambayo imewawezesha kufanya vizuri katika mtihani wao.

Pamoja na watahiniwa wengi kufanya vizuri katika mtihani wa Maarifa ya Jamii, wapo watahiniwa wachache walioshindwa kujibu vizuri baadhi ya maswali. Sababu zilizobainika kusababisha watahiniwa hao kushindwa kujibu maswali kwa ufasaha ni pamoja na:kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika, kutoelewa matakwa ya maswali na hivyo kutoa majibu ambayo hayakujibu maswali waliyoulizwa, kutokuwa makini katika kusoma maswali hivyo kuwafanya watoe majibu ambayo hayakuendana na matakwa ya swali, kushindwa kuhawilisha maarifa ya dhana moja na nyingine pamoja na kuchanganya dhana na hivyo, kutoa majibu ambayo hayakuwa yamekusudiwa na maswali husika.

Ni matarajio ya Baraza la Mitihani la Tanzania kuwa, taarifa hii itatoa mrejesho ambao utatumiwa na wadau mbalimbali katika kuboresha mafunzo ya masomo ya Historia na Jiografia katika ngazi ya cheti na pia kushughulikia kasoro zilizobainishwa ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji katika vyuo vya Elimu na

hivyo, kuwezesha kutoa walimu bora wa somo la Maarifa ya Jamii na kuboresha kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa tarajali.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii ya Mtihani wa Maarifa ya Jamii, Ualimu Daraja la A mwaka 2018 inachambua viwango vya kufaulu kwa watahiniwa kwa lengo la kutoa mrejesho kuhusu namna watahiniwa walivyojibu maswali katika mtihani huo.

Maswali ya mtihani wa 614 Maarifa ya Jamii yanatokana na mada za masomo ya Jiografia na Historia yanayofundishwa katika ngazi ya cheti. Mtihani wa Maarifa ya Jamii ulikuwa na jumla ya maswali kumi na sita (16) yaliyogawanywa katika sehemu A, B na C. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali kumi na nne (14) ambapo sehemu A walitakiwa kujibu maswali kumi (10), maswali matano (5) ya somo la Jiografia na maswali matano (5) ya somo la Historia. Sehemu B ilikuwa na maswali ya insha yaliyogawanyika katika vipengelele viwili (2) kutoka katika mada za taaluma za masomo ya Jiografia na Historia. Mtahiniwa alitakiwa kujibu swali moja (1) kutoka katika kipengele cha Jiografia na swali moja (1) kutoka katika kipengele cha Historia. Sehemu C ilikuwa na maswali mawili kutoka katika mada za ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Jiografia na Hisitoria. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu hii.

Mtihani huu wa Maarifa ya Jamii, Ualimu ngazi ya Daraja A 2018 ulifanywa na jumla ya watahiniwa 4,843 ambao ni sawa na asilimia 98.8 ya watahiniwa 4,900 waliosajiliwa kufanya mtihani huo. Kiwango cha ufaulu katika mtihani huu kilikuwa kizuri, kwani asilimia 99.98 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani Maarifa ya Jamii walifaulu.

Ufaulu wa watahiniwa umegawanywa katika makundi matatu kutegemea alama walizopata watahiniwa katika swali. Aidha, sababu za watahiniwa kujibu vizuri au kushindwa kujibu vizuri zimeainishwa kwa uthibitisho. Sampuli za majibu ya watahiniwa zimetumika kama vielelezo ili kuwawezesha wadau mbalimbali kuona mifano ya hoja zinazotolewa.


## 2.0 TATHMINI YA MAJIBU YA MTAHINIWA KWA KILA SWALI

## 2.1 SEHEMU A: TAALUMA

Sehemu A ya mtihani wa Maarifa ya Jamii ilikuwa na maswali 10 ya majibu mafupi. Kila swali katika sehemu hiyo lilikuwa na jumla ya alama nne (4). Kufaulu kwa watahiniwa katika sehemu hii kuligawanywa katika makundi matatu kulingana na alama walizopata watahiniwa. Watahiniwa waliopata kati ya alama 0 hadi 1.5 walihesabika kuwa na ufaulu hafifu katika swali husika. Watahiniwa waliopata alama kati ya 2 hadi 2.5 walihesabika kuwa na ufaulu wa wastani,na iwapo walipata alama kati ya 3 hadi 4 walihesabika kuwa na ufaulu mzuri.

### 2.1.1 Swali 1. Sayari Dunia

Swali la 1 lilitoka katika mada ya Sayari Dunia. Mtahiniwa katika swali hili alitakiwa kubainisha matokeo manne yanayotokana na mizunguko ya dunia. Watahiniwa 4,843 (100%) walijibu swali hili. Watahiniwa 65 (1.3%) walipata alama kati ya 0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu hafifu. Pia watahiniwa 393 (8.1%) walipata alama kati ya 2 hadi 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani. Watahiniwa 4,387 (90.6%) walijibu swali hilo vizuri kwa kupata alama kati ya 3 hadi 4. Kwa ujumla, watahiniwa walifaulu vizuri katika swali hili kwani jumla ya watahiniwa 4,780 (98.7%) walipata alama kati ya 2 hadi 4 ambazo ziliwawezesha kufaulu swali hilo. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 1.





**Chati Na.1**: Inaonesha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 1.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, watahiniwa wengi walikuwa na ufahamu mzuri kuhusu matokeo ya mizunguko ya dunia suala ambalo liliwawezesha kujibu swali kwa ufasaha.

Aidha, ushahidi katika majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa walijibu vizuri kutokana na uelewa wa matakwa ya swali na hivyo kuthibitisha kuwa, mada ya sayari dunia ilieleweka vizuri wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Watahiniwa waliweza kubainisha matokeo ya mizunguko ya dunia kama vile kutokea kwa usiku na mchana, mabadiliko ya jua la utosi, tofauti ya urefu wa usiku na mchana, kutokea kwa majira mbalimbali ya mwaka, tofauti ya mawio na machweo pamoja na kupinda kwa mikondo ya bahari. Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi na kupata alama zote kwani alibainisha matokeo yanayotokana na mizunguko ya dunia na kutoa maelezo mafupi.

**Kielelezo Na.1.1 Sampuli ya Jibu zuri la Mtahiniwa**



1 Kuna mizunguko mikuu miwili ya dunia nayo ni
(i) dunia kujizungusha katika mhimili wake
(ii) dunia kuzunguka jua.

matokeo ya mizunguko ya dunia ni.
(i) Kutokea kwa usiku na mchana, dunia inapojizungusha katika mhimili wake upande unaoelekea jua hupata mchana na upande wa pili huwa usiku.

(ii) Kutokea kwa majira ya mwaka, dunia inazunguka jua kwa muda wa siku 365 au 366, sawa na mwaka mmoja. hivyo majira kama kiangazi, vuli, masika hutokea


(iii) Tofauti ya urefu wa usiku na mchana, siku zote usiku na mchana hazifanani, siku zinazofanana ni zile ambazo jua huwa la utosi kwenye ikweta tar 21, machi na tarehe 23, septemba.

(iv) Tofauti ya jua la utosi, dunia inapozunguka jua huwa kunatokea jua la utosi katika nyakati mbali mbali. mfano tarehe 21 machi na 23, septemba jua huwa la utosi kwenye ikweta, tarehe 21, juni jua huwa la utosi kwenye tropiki ya kansa na tarehe 22, desemba jua huwa la utosi kwenye tropiki ya kaprikoni

**Kielelezo Na. 1.1:** Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyekidhi matakwa ya swali kwa kueleza kwa kifupi matokeo mizunguko ya dunia.

Kwa upande mwingine, ufaulu hafifu ulisababishwa na watahiniwa kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu matokeo ya mizunguko ya dunia. Baadhi yao walitaja misimu mbalimbali ya majira ya mwaka ambayo kimsingi ilikuwa ni hoja mojawapo tu kati ya zile zilizotakiwa. Kwa mfano, watahiniwa wengine walichanganya dhana za matokeo ya mizunguko ya dunia na matokeo yatokanayo na mzunguko wa mwezi kuizunguka dunia ambayo ni kupatwa kwa mwezii na kupatwa kwa jua. Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa majibu yasiyotosheleza matakwa ya swali.

**Kielelezo Na. 1.2**


1. Matokeo manne yanayotokana na mizunguko wa dunia ni:-
i) Masika
ii) Kiangazi
iii) Kipupwe
iv) Michipuko


**Kielelezo Na. 1.2:** Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye hakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu matokeo ya mizunguko ya dunia na hivyo kuorodhesha misimu katika mwaka ambayo kimsingi ni hoja moja.

### 2.1.2 Swali 2. Nchi yetu Tanzania

Swali la 2 lilitoka katika mada ya Nchi yetu Tanzania. Katika swali hilo mtahiniwa alitakiwa kupendekeza na kisha kueleza kwa kifupi mbinu nne zinazoweza kutumika katika kukabiliana na changamoto zinazotokana na makazi holela. Swali hilo lililenga kupima nyanja ya matumizi ambapo mtahiniwa alitakiwa kutumia maarifa aliyonayo kuhusu changamoto za makazi holela ambayo yangemwezesha kutoa mapendekezo yanayoweza kupunguza tatizo hilo.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walijibu swali hili. Watahiniwa 662 (13.7%) walipata alama kati ya 0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu hafifu**.** Pia watahiniwa 607 (12.5%) walipata alama kati ya 2 hadi 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani. Watahiniwa 3,575 (73.8%) walijibu swali hilo vizuri kwa kupata alama kati ya 3 hadi 4. Kwa ujumla, watahiniwa walifaulu


vizuri katika swali hili kwani jumla ya watahiniwa 4,182 (86.3%) walipata alama kati ya 2 hadi 4 ambazo ziliwawezesha kufaulu swali hilo. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na. 2.




**Chati Na.2**: Inaonesha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 2.

Ufaulu huu mzuri katika swali hili, ulitokana na uelewa wa watahiniwa wa mahitaji ya swali na ufahamu kuhusu athari za makazi holela katika mazingira na maisha yao ya kila siku hivyo, kuwawezesha kupendekeza na kueleza mbinu sahihi za kukabiliana na changamoto za makazi holela. Mathalani, watahiniwa walioweza kujibu vizuri swali hili waliweza kutoa mapendekezo kama vile kuanzisha makazi mapya yaliyopangwa, kupima maeneo na kusimamia ujenzi, kuboresha huduma za kijamii vijijini na mijini ili kupunguza msongamano mijini ambako huwa kuna huduma hizo, kutoa elimu ya mazingira kwa wananchi pamoja na kutunga sheria ndogondogo zinazolenga kulinda mazingira na kuboresha makazi. Kielelezo Na. 1.3 ni sampuli inayothibitisha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo Na. 1.3**


02. i/ Mipango miji / Vijiji. Serikali inatakiwa kuweka mipango katika vijiji au miji ya namna ya kukaa.

ii/ Elimu. Elimu itolewe kwa kutaja changamoto zinazotokana na makazi holela ya watu


iii/ Serikali iweze kusimamia pindi wakazi wanapoanza kujenga ili kujiridhisha.

iv/ Kuwepo kwa sheria ambayo itatumiwa kwa wale watakaosababisha makazi holela.

**Kielelezo Na. 1.3:** Kinaonesha sampuli ya jibu la Mtahiniwa aliyeweza kupendekeza hatua sahihi zinazoweza kuchukuliwa ili kukabiliana na changamoto ya makazi holela.

Aidha, ufaulu hafifu ulitokana na watahiniwa kutoelewa mahitaji ya swali na kutokuwa makini jambo lililowafanya watoe majibu ambayo hayakuendana na matakwa ya swali. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walieleza mbinu za ufundishaji badala ya kueleza mbinu za kukabiliana na changamoto za makazi holela. Baadhi ya watahiniwa walitoa mapendekezo ambayo hayakuwa na uhusiano wa moja kwa moja na utatuzi wa changamoto za makazi holela kama vile, ujenzi wa nyumba bora na za kudumu, kuanzisha biashara  na kupanda miti ya kivuli na matunda, hatua ambazo hazilengi kutatua changamoto ya makazi holela. Kielelezo Na. 1.4 ni sampuli yenye ushahidi wa majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.

**Kielelezo Na. 1.4**


2. i) Mhadhara:
- mbinu ya mhadhara inaweza kutumika katika kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazotokana na makazi kwa sababu ya kueleza na kutaka kufahamu kwa nini changamoto zinajitokeza katika sehemu hiyo.


ii) Mahojiano:
Pia kwa kutoa watu mbalimbali katika eneo ambalo kuna changamoto na kuwauliza maswali ambayo yatakusaidia kujua namna ya kutatua changamoto hizo kwa sababu ambazo utakuwa umeelezwa na nini chanzo cha changamoto hizo.

**Kielelezo Na. 1.4:** Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye hakuzingatia matakwa ya swali kwa kueleza mbinu za kufundishia na kujifunzia badala ya kupendekeza mbinu zinazoweza kutumika kutatua changamoto za makazi holela

### 2.1.3 Swali 3: Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani

Swali la 3 lilitoka katika mada ya Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani. Swali lilikuwa na vipengele viwili; Katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kifupi dhana ya kipimo cha ramani. Kipengele hiki cha swali kililenga kupima nyanja ya maarifa kuhusu dhana ya kipimo cha ramani. Katika kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kutoa ufafanuzi mfupi wa njia tatu zinazoweza kutumika katika kuonesha kipimo cha ramani. Kipengele hiki kililenga kupima nyanja ya ufahamu.


Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walijibu swali hili. Watahiniwa 719 (14.8%) walipata alama kati ya 0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu hafifu. Pia, watahiniwa 365 (7.6%) walipata alama kati ya 2 hadi 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani. Watahiniwa 3,760 (77.6%) walijibu swali hilo vizuri kwa kupata alama kati ya 3 hadi 4. Kwa ujumla, watahiniwa walifaulu vizuri katika swali hili kwani jumla ya watahiniwa 4,125 (85.2%) walipata alama kati ya 2 hadi 4 ambazo ziliwawezesha kufaulu swali hilo. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na. 3.




**Chati Na.3**: Inaonesha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 3.

Watahiniwa waliweza kujibu swali hili kwa usahihi kutokana na swali kuwa wazi na hivyo, kuwawezesha watahiniwa kuelewa matakwa ya swali kwa urahisi na watahiniwa kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada husika. Kielelezo Na. 1.5 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili kwani aliweza kueleza dhana ya kipimo na kufafanua njia zinazoweza kutumika katika kuonesha kipimo cha ramani ambazo ni njia ya maneno, njia ya mstari na njia ya uwiano.

**Kielelezo Na. 1.5**


3 (a) Kipimio cha ramani
Ni kielelezo kinachotumika kuonyesha uhusiano uliopo kati ya ramani iliyochorwa na umbali katika ardhi.

3 (b) Njia za kuonyesha kipimio
i) kwa njia ya maelezo.
mfano sentimita mbili katika ramani huwakilisha kilomita moja katika ardhi.


ii) kwa njia ya uwiano au sehemu
mfano 1:50,000 au 1/50,000

iii) kwa njia ya mstari.
kwa kulinganisha aina ya uwiano uliopewa na kuubadili kuwa katika sm. mfano km 7½ utaibadili iwe katika sm ambayo ni sawa na sentimita 5 na meta 1000

**Kielelezo Na. 1.5:** Kinaonesha sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa ambaye aliweza kueleza kwa kifupi dhana ya kipimo cha ramani ma kuieleza kwa usahihi njia tatu zinazoweza kutumika kuwasilisha kipimo cha ramani.

Aidha, baadhi ya watahiniwa walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi na hata baadhi yao kupata alama 0. Hii ni kutokana na watahiniwa kutoelewa matakwa ya swali, hivyo kueleza mambo yasiyohusiana na majibu ya swali. Hii inadhihirisha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa dhana ya kipimo cha ramani pamoja na njia zinazotumika katika kuonesha kupimo cha ramani. Kielelezo Na. 1.6 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili kwani alitaja njia za kiikweta, kitropki na kisavana badala ya njia sahihi zinazotumika kuonesha kipimo cha ramani.

**Kielelezo Na. 1.6**



3 a. Kipimo cha ramani:
Hiki ni kipimo kinachotumika kuigawa ramani katika pande tuu nne za dunia.
b. ⇒ Njia ya kiikweta
⇒ Njia ya kitropiti
⇒ Njia ya kisavana

**Kielelezo Na. 1.6:** Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye hakuwa na uelewa wa mahitaji ya swali, na hivyo kutoa dhana isiyo sahihi ya kipimo cha ramani na kuorodhesha njia zisizo sahihi kama Kiikweta, Kaprikoni na Kisavana.

### 2.1.4 Swali 4. Nchi Yetu Tanzania

Swali la 5 lilitoka katika mada ya Nchi Yetu Tanzania. Swali lililenga kupima nyanja ya matumizi. Mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kifupi manufaa ya kiuchumi yatokanayo na maumbile ya nchi yanayopatikana nchini Tanzania.


Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walijibu swali hili. Watahiniwa 44 (0.8%) walipata alama kati ya 0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu hafifu. Pia, watahiniwa 68 (1.4%) walipata alama kati ya 2 hadi 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani.Watahiniwa 4,732 (97.8%) walijibu swali hilo vizuri kwa kupata alama kati ya 3 hadi 4. Kwa ujumla, watahiniwa walifaulu vizuri katika swali hili kwani jumla ya watahiniwa 4,800 (99%) walipata alama kati ya 2 hadi 4 ambazo ziliwawezesha kufaulu swali hilo. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na. 4.




**Chati Na.4**: Inaonesha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 4.

Watahiniwa walifanya vizuri katika swali hili kutokana na kuwa na uelewa mzuri wa maumbile ya nchi yao hasa yanayopatikana katika mazingira wanayoishi. Vilevile, majibu ya watahiniwa yanaonesha walielewa vizuri mada ya Nchi Yetu Tanzania wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Watahiniwa waliweza kueleza manufaa mbalimbali kama vile usafirishaji, vivutio vya utalii, vyanzo vya madini, uvuvi, uzalishaji wa umeme na vyanzo vya maji. Kielelezo Na. 1.7 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo Na. 1.7**



4 Maumbile ya nchi yanayopatikana nchini Tanzania ni pamoja na milima, uoto wa asili, mabonde, mito, maziwa na bahari yana manufaa yafuatayo:

i) Husaidia nchi kupata fedha za kigeni nchi hupata fedha za kigeni kupitia watu ambao hufika nchini na kuhitaji kuangalia maumbile hayo mfano mlima kilimanjaro pia hutoa fedha ili wahudumiwe

ii) Huvutia watalii; maumbile ya nchi yamekuwa ~~kit~~ kivutio kikubwa sana cha watalii kutoka nchi mbali mbali ambao hufika na kujionea sio bure bali kwa kutoa fedha kama malipo.


4 iii) Hukuza uchumi wa nchi, maumbile
haya husaidia kukuza uchumi wa nchi
kwasababu watu hupata malighafi zito
kanazo na maumbile ya nchi na kuuza
mfano wa malighafi ni Samaki, ~~pdau~~ pia
hufanya kilimo katika mabonde.

iv) Husaidia kuzalisha umeme ambao hus
idia kuzalisha shughuli za kiuchumi
na nchi hujikuta uchumi ukiongezeka
siku hadi siku.

**Kielelezo Na. 1.7:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahihiwa ambaye alieleza kwa kifupi manufaa ya kiuchumi yatokanayo na maumbile ya nchi.

Licha ya watahiniwa wengi kujibu swali hili vizuri, watahiniwa wachache (0.9%) walishindwa kujibu swali kwa usahihi na hata baadhi yao kutopata alama yoyote. Sababu ya kujibu vibaya swali hili ni watahiniwa kutokuwa na ufahamu wa dhana ya manufaa ya kiuchumi pamoja na uhusiano wake na maumbile au sura ya nchi. Watahiniwa hao pia hawakuwa na uelewa wa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu ambayo hayahusiani kabisa na mahitaji ya swali kwa kuelezea mistari ya Ikweta, Greenwich, Longitudo na Latitudo badala ya kueleza manufaa manne ya kiuchumi yatokanayo na maumbile ya nchi yanayopatikana nchini Tanzania. Kielelezo Na. 1.8 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.

**Kielelezo Na. 1.8**



4 Manufaa ya kiuchumi yatokanayo na maumbile ya nchi yanayopatikana nchini Tanzania.

(i) Ikweta

Ni msitari Unaoigawa dunia katika sehemu mbili yaani Kaskazini na kusini. Inasaidia kuangalia pande kuu za dunia.

(ii) Greenwich

Ni mstari Unaoigawa dunia katika sehemu mbili magharibi na mashariki.

iii) Longitudo


iv) Latitudo.

**Kielelezo Na. 1.8:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakuzingatia matakwa ya swali kwa kueleza baadhi ya mistari ya longitudo na latitudo badala ya manufaa ya kiuchumi yanayotokana na maumbile au sura ya nchi.

### 2.1.5 Swali 5. Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani

Swali la 5 lilitoka katika mada ya Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani**.** Swali lililenga kupima majazi ya utambuzi ngazi ya uchambuzi. Mtahiniwa katika swali hili alitakiwa kufafanua kwa kifupi kazi ya vipengele vinne vya ramani kwa kuzingatia vipengele vinavyounda ramani.


Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walijibu swali hili. Watahiniwa 176 (3.6%) walipata alama kati ya 0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu hafifu. Pia, watahiniwa 12 (2.6%) walipata alama kati ya 2 hadi 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani. Watahiniwa 4,541 (93.7%) walijibu swali hilo vizuri kwa kupata alama kati ya 3 hadi 4. Kwa ujumla, watahiniwa walifaulu vizuri katika swali hili kwani jumla ya watahiniwa 4,668 (96.3%) walipata alama kati ya 2 hadi 4 ambazo ziliwawezesha kufaulu swali hilo. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na. 5.




**Chati Na. 5**: Inaonesha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 5.

Watahiniwa walifanya vizuri katika swali hili kutokana na swali kuwa wazi na hivyo, kuwawezesha watahiniwa kuelewa matakwa ya swali kwa urahisi. Pia, majibu ya watahiniwa yalidhihirisha kuwa, mada ya Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani ilieleweka vizuri kwa wanachuo wengi wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Watahiniwa waliweza kueleza vizuri matumizi ya vipengele vya ramani kama vile, kichwa cha habari cha ramani, kipimo, dira, pamoja na ufunguo. Kielelezo Na. 1.9 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili kwa kuonyesha kipengele cha ramani na kutoa ufafanuzi mfupi kuhusu matumizi ya kila kipengele.


**Kielelezo Na. 1.9**


05. Kufafanua kazi ya vipengele vinavyounda ramani:
i/. Kichwa cha Ramani; hiki ni kitu cho ueleza ramani ni kwa ajili ya nini na ni ramani ya wapi. mfano. RAMANI YA TANZANIA KUONESHA UTALII.
ii/. Ufunguo; ni kitu cho kipengele kinachotumia alama na michoro mbalimbali kuonesha mambo yaliyomo kwenye ramani. mfano, kuwakilisha almasi (madini). kuwakilisha barabara.
iii/. Skeli: ni kipimo kinachoambatana kwa mfumo wa uwiano kikiwakilisha vipimo vya ramani kwenye mchoro wake na kulinganisha kwenye ardhi. mfano, ramani yenye vipimo vya 1:500,000
iv/. Dira ni kipengele kinachoonesha uelekeo wa ramani kwa kuonesha upande wa kaskazini na pande nyingine. mfano.

**Kielelezo Na. 1.9:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alijibu vizuri swali hili kwa kuonyesha vipengele vya ramani na kutoa ufafanuzi mfupi kuhusu matumizi ya kila kipengele.

Pamoja na watahiniwa wengi kujibu swali hili kwa ufasaha, wapo watahiniwa wachache waliofanya mtihani huu walijibu vibaya swali hili na baadhi yao kupata alama 0. Watahiniwa walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi kutokana na kuchanganya dhana pamoja na kutoelewa matumizi ya vipengele vya ramani, hivyo kusababisha kutoa majibu ambayo hayana uhusiano na swali, na hivyo kufaulu kwa kiwango hafifu. Kielelezo Na. 1.10 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili kwa kutoa majibu ambayo hayana uhusiano kabisa na swali kwa kuchanganya sura ya nchi na vipengele vya ramani.

**Kielelezo Na. 1.10**



5. i/ MILIMA
~~Ni muinuko unaotenganisha bonde~~
~~Kutenganisha mabonde~~
- Kuonesha mistari ya kontua
ii/ GENGE
- Kuonesha mistari ya longitude na latitude iliyopita.
iii/ PITO
- Kuonesha mistari ya kontua
iv/ MTO
- Kuonesha umbali na usawa wa bahari

**Kielelezo Na. 1.10:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakuzingatia matakwa ya swali kwani alitoa majibu ambayo hayana uhusiano kabisa na swali kwa kuchanganya sura ya nchi na vipengele vya ramani.

### 2.1.6 Swali 6. Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika

Swali la 6 lilitoka katika mada ya Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika. Swali hili lililenga kupima nyanja ya ufahamu. Mtahiniwa alipaswa kutoa sababu nne kwa kifupi za Wamisionari kujihusisha katika kupinga biashara ya utumwa barani Afrika.


Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walijibu swali hili. Watahiniwa 826 (17.1%) walipata alama kati ya 0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu hafifu. Pia, watahiniwa 768 (15.8%) walipata alama kati ya 2 hadi 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani. Watahiniwa 3,250 (67.1%) waliweza kujibu swali hilo vizuri kwa kupata alama kati ya 3 hadi 4. Kwa ujumla, watahiniwa walifaulu vizuri katika swali hili kwani jumla ya watahiniwa 4,018 (82.9%) walipata alama kati ya 2 hadi 4 ambazo ziliwawezesha kufaulu swali hilo. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na. 6.




**Chati Na. 6**: Inaonesha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 6.

Watahiniwa walifanya vizuri katika swali hili kutokana na swali kuwa la wazi na hivyo, kuwafanya watahiniwa kuelewa matakwa ya swali kwa urahisi. Watahiniwa waliojibu vizuri swali hilo waliweza kueleza sababu mbalimbali, kwa mfano; kuwapumbaza waafrika ili wasipinge ukoloni, kuwastaarabisha waafrika, kupata nguvu kazi au watu wa kuweza kuwatumikia pamoja na kuanzisha dini mpya (Ukristo). Kielelezo Na. 1.11 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo Na. 1.11**


06 Sababu za wamisionari kujihusisha katika kupinga biashara ya utumwa barani Afrika ni kama zifuatazo:-

Ili kuwa ni kinyume na haki za binadamu, wamisionari walikuwa ni watu wenye Imani ya dini ya kikristo hivyo Imani ya dini yao inawakataza kunyanyasa haki ya binadamu wengine na uzalilishaji.

Walihitaji kupata watu wa kuweza kuwatumikia ili kufikia malengo yao, hivyo biashara ya utumwa ilipunguza idadi ya watu na nguvu kazi ambayo w. walihitaji.


Pia walitaka kuwalainisha waafrika, ili waafrika waweze kuwapokea na kuwaona kuwa wao ni watu wema hivyo walitumia mbinu hii ili waweze kuwatawala kirahisi hapo baadae.

Walikuja kwa lengo la kuwastaarabisha waafrika, wakati wanafika walikuta waafrika wanamila na tamaduni ambazo kwao zilikuwa mbaya lakini ndani yake walikuta waarabu wakifanya utaratibu huu ambao kwao pia haukuwa ndani ya ustaarabu wa mataifa yao hivyo wakaichukua kama sehemu ya kushughulikia ili kuleta ustarabu barani afrika.

**Kielelezo Na. 1.11:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alielewa matakwa ya swali na kuweza kueleza sababu mbalimbali zikiwemo; kupata nguvu kazi au watu wa kuweza kuwatumikia, kuwapumbaza waafrika ili wasipinge ukoloni, kuwastaarabisha Waafrika na kuanzisha dini mpya.

Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa wachache walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi na kupata alama chini ya wastani. Hii ilisababishwa na watahiniwa hawa kutofuata maelekezo ya swali kwani baadhi yao walitoa tu

sababu bila kutoa maelezo mafupi na wengine walitoa majibu yasiyoendana kabisa na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 1.12 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya katika swali hili.



6 i/ Ili kukuza uchumi wa waafrika
ii/ Ili kuongeza idadi ya watu katika Afrika
iii/ Ili kuwafanya waafrika kuwa huru
iv/ Ili kuimarisha na kuboresha huduma za kiafrika

**Kielelezo Na. 1.12:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alitoa majibu yasiyoendana kabisa na matakwa ya swali.

### 2.1.7 Swali 7. Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika

Swali la 7 lilitoka katika mada ya Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika. Swali hilo lililenga kupima nyanja ya ufahamu. Mtahiniwa katika swali hili alitakiwa kutumia mifano kubainisha hatua nne zilizochukuliwa na Waingereza katika kuimarisha uchumi wa kikoloni katika koloni la Tanganyika.


Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walijibu swali hili. Watahiniwa 1,782 (36.8%) walipata alama kati ya 0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu hafifu. Pia, watahiniwa 1,251 (25.8%) walipata alama kati ya 2 hadi 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani. Watahiniwa 1,811 (37.4%) walijibu swali hilo vizuri kwa kupata alama kati ya 3 hadi 4. Kwa ujumla, watahiniwa walifaulu vizuri katika swali hili kwani jumla ya watahiniwa 3,062 (63.2%) walipata alama kati ya 2 hadi 4 ambazo ziliwawezesha kufaulu swali hilo. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na. 7.




**Chati Na. 7**: Inaonesha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 7.

Watahiniwa walijibu swali hili vizuri kutokana na kuelewa mahitaji ya swali na kuweza kubainisha kwa usahihi hatua zilizochukuliwa na Waingereza katika kuimarisha uchumi wa kikoloni katika koloni la Tanganyika. Kielelezo Na. 1.13 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.


**Kielelezo Na. 1.13**


7. (i) Kuwalipisha kodi waafrika mfano kodi ya kibanda
(ii) Kuanzishwa kwa viwanda mfano viwanda vya-
usindikaji.
(iii) Kuanzishwa kwa matumizi ya fedha mfano kuo-
ndoa matumizi ya kubadilishana bidhaa kwa bidhaa
(iv) Kuimarisha na kuboresha miundombinu mfano reli,
barabara na bandari.

**Kielelezo Na. 1.13:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alikuwa na maarifa ya kutosha ya swali kwani aliweza kubainisha hatua zilizotumika na Waingereza kuimarisha uchumi wa kikoloni.

Aidha, watahiniwa wachache waliofanya upimaji huu walipata ufaulu hafifu kwa kuwa walishindwa kujibu swali kwa usahihi kutokana na kutoelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walibainisha hatua zilizochukuliwa na Waingereza katika kuimarisha utawala wa kikoloni Tanganyika badala ya kubainisha hatua zilizochukuliwa na Waingereza katika kuimarisha uchumi wa kikoloni Tanganyika. Kielelezo Na. 1.14 ni

sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika mbinu zilizotumika kuanzisha ukoloni badala ya njia zilizotumika kuimarisha uchumi wa kikoloni Tanganyika.



7 i) Kuungana na jamii au makabila dhaifu mfano
ii) Kufanya mikataba na viongozi wa makabila mfano Chief mangungo na Karl peter.
iii) Kufanya vitendo vya mauaji na mateso hazarani
iv) Udanganyifu.

**Kielelezo Na. 1.14:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakuwa makini kuelewa mahitaji ya swali ambapo alibainisha hatua zilizochukuliwa kuimarisha utawala wa kikoloni Tanganyika badala ya hatua za kuimarisha uchumi wa kikoloni Tanganyika.

### 2.1.8 Swali 8. Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi katika Afrika Huru

Swali la 8 lilitoka katika mada ya Mabadiliko ya Kijammii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika Huru. Swali hili lililenga kupima ufahamu wa mtahiniwa kuhusu mafanikio mawili ya kiuchumi na mafanikio mawili ya kijamii yaliyofikiwa na nchi za Afrika baada ya uhuru.


Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walijibu swali hili. Watahiniwa 875 (18.1%) walipata alama kati ya 0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu hafifu. Pia, watahiniwa 994 (20.5%) walipata alama kati ya 2 hadi 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani. Watahiniwa 2,975 (61.4%) walijibu swali hilo vizuri kwa kupata alama kati ya 3 hadi 4. Kwa ujumla, watahiniwa walifaulu vizuri katika swali hili kwani jumla ya watahiniwa 3,969 (81.9%) walipata alama kati ya 2 hadi 4 ambazo ziliwawezesha kufaulu swali hilo. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na. 8.




**Chati Na. 8**: Inaonesha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 8.

Watahiniwa waliweza kujibu vizuri swali hili kutokana na kuelewa mahitaji ya swali na hivyo, kuweza kubainisha mafaniko ya kiuchumi na kijamii yaliyofikiwa na nchi za Afrika baada ya uhuru. Kielelezo 1.15 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.


**Kielelezo Na. 1.15**


8. mafaniko ya kiuchumi:-
a, kukua kwa viwanda barani Afrika
mfano nchi ya Afrika kusini
b kuboreshwa kwa miundombinu na
njia za usafirishaji wa bidhaa.
mfano uwepo wa reli za umeme na
barabara bora za viwango vya lami
katika nchi za kiafrika mfano nchi
ya Naigeria
mafaniko ya kijamii
i, Upatikanaji wa huduma bora za kija-
mii mfano huduma za Afya, maji, Elimu
ii, Upatikanaji wa makazi bora na ya
kudumu.

**Kielelezo 1.15:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyekidhi matakwa ya swali na hivyo, kubainisha kwa ufasaha mafaniko ya kiuchumi na kijamii yaliyofikiwa na nchi za Afrika baada ya uhuru.

Hata hivyo, watahiniwa wachache walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi kutokana na kutokuwa makini wakati wa kujibu swali na kutoelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walibainisha mafanikio ya kisiasa tofauti na matakwa ya swali yaliyowataka wabainishe mafanikio ya kiuchumi na kijamii yaliyofikiwa na nchi za Afrika baada ya uhuru. Kielelezo Na. 1.16 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.

**Kielelezo Na. 1.16**


8. Mafanikio ya Kiuchumi yaliyofanikiwa kth Afrika baada ya Uruhu.
> Biashara.
> Ushirikiano wa Kimataifa.

Kijamii.
> Ulinzi na usalama.
> Mfumo wa siasa.


**Kielelezo 1.16:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakuzingatia matakwa ya swali kwani alibainisha mafanikio ya kisiasa tofauti na matakwa ya swali yaliyomtaka abainishe mafanikio ya kiuchumi na kijamii yaliyofikiwa na nchi za Afrika baada ya uhuru.

### 2.1.9 Swali 9. Ushirikiano wa Kimataifa

Swali la 9 lilitoka katika mada ya Ushirikiano wa Kimataifa na lililenga kupima nyanja ya ufahamu. Mtahiniwa alipaswa kueleza kwa ufupi malengo makuu ya kuundwa kwa Umoja wa Mataifa.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walijibu swali hili. Watahiniwa 221 (4.6%) walipata alama kati ya 0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu hafifu. Aidha, watahiniwa 443 (9.1%) walipata alama kati ya 2 hadi 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani. Watahiniwa 4,180 (86.3%) waliweza kujibu swali hilo vizuri kwa kupata alama kati ya 3 hadi 4. Kwa ujumla, watahiniwa walifaulu vizuri katika swali hili kwani jumla ya watahiniwa 4,623 (95.4%) walipata alama kati ya 2 hadi 4 ambazo ziliwawezesha kufaulu swali hilo. Muhtasari wa


kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na. 9.




**Chati Na. 9**: Inaonesha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 9.

Watahiniwa walifaulu vizuri swali hili kutokana na swali kuwa wazi kiasi cha kuwafanya watahiniwa kuelewa matakwa ya swali kwa urahisi. Kielelezo Na. 1.17 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kieelelezo Na. 1.17**



9. i/ Kudumisha ulinzi na usalama miongoni mwa nchi wanachama

ii/ Kuendeleza urafiki na ushirikiano miongo mwa nchi wanachama.


iii/ Kutoa huduma au msaada wa kibinadamu yanapotokea majanga miongoni mwa nchi wanachama.

iv/ Kusaidia nchi wanachama kukuza uchumi wake

**Kielelezo 1.17:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alizingatia matakwa ya swali na akaweza kueleza kwa ufupi malengo makuu ya kuundwa kwa Umoja wa Mataifa.

Licha ya watahiniwa wengi kujibu vizuri swali hili, watahiniwa wachache walishindwa kujibu swali kwa usahihi kutokana na kutoelewa swali, hivyo kuchanganya majibu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza malengo ya Umoja wa Afrika badala ya kueleza malengo makuu ya kuundwa kwa Umoja wa Mataifa. Kielelezo Na. 1.18 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.

**Kielelezo Na. 1.18**


9. Malengo [illegible] makuu ya kuundwa AU
(i) Kuendeleza amani katika umoja wa Afrika
(ii) Kutatua migogoro, mapinduzi ya umoja wa wa Afrika
(iii) Kulinda haki na [illegible]
(iv) Kukuza ushirikiano baina ya nchi za Umoja wa Afrika


**Kielelezo 1.18:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakuelewa matakwa ya swali hivyo kuchanganya majibu na kueleza malengo ya Umoja wa Afrika badala ya kueleza malengo makuu ya kuundwa kwa Umoja wa Mataifa.

### 2.1.10 Swali 10. Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika Huru

Swali la 10 lilitoka katika mada ya Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika Huru. Swali hili lililenga kupima nyanja ya tathmini na mtahiniwa alipaswa kutumia mifano kutathmini kwa ufupi athari nne za migogoro ya kisiasa katika nchi za Afrika.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walijibu swali hili. Watahiniwa 416 (8.6%) walipata alama kati ya 0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu hafifu. Pia, watahiniwa 944 (19.5%) walipata alama kati ya 2 hadi 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani. Watahiniwa 3,483 (71.9%) waliweza kujibu vizuri swali hili kwa kupata alama kati ya 3 hadi 4. Kwa ujumla, watahiniwa walifaulu vizuri katika swali hili kwani jumla ya watahiniwa 4,427 (91.4%) walipata alama


kati ya 2 hadi 4 ambazo ziliwawezesha kufaulu swali hilo. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na. 10.




**Chati Na. 10**: Inaonesha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 10.

Sababu ya kujibu swali hili vizuri ni kutokana na watahiniwa kuelewa matakwa ya swali, na hivyo kutoa mifano halisi katika kufanya tathmini ya migogoro ya kisiasa katika nchi za Afrika. Kielelezo Na. 1.19 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo Na. 1.19**



10. (i). Hupelekea Vifo
- Hii husababishwa na chuki zinazokuwepo baina ya pande zinazokinzana ambapo watu wengi huuawa kutokana na ushabiki au kutetea chama mojawapo cha kisiasa.

(ii). Hupelekea Mtawanyiko wa watu.
- Hii husababishwa na watu kuyakimbia makazi yao maalumu kwa kuokoa uhai, hii kutokana na kuhitilafiana kwa Vyama mbalimbali vya kisiasa. Mfano, katika nchi ya Kenya ambako uchaguzi huleta shida na kupelekea watu kuyakimbia makazi yao.


(iii). Kuongezeka kwa Makundi ya kihalifu
- Watu wengi hujihusisha na wizi, uporaji, utekaji kutokana na kushinikizwa kufanya vitendo vya kiovu na viongozi mbalimbali wa kisiasa.

(iv). Husababisha Vita Vya Wenyewe kwa Wenyewe.
- Hii ni kutokana na kuwepo ~~kwa tofauti~~ baina ya Makundi mbalimbali ya Vyama.

**Kielelezo Na. 1.19:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alizingatia matakwa ya swali, hivyo kutoa mifano halisi katika kufanya tathmini ya migogoro ya kisiasa katika nchi za Afrika.

Aidha, watahiniwa wachache (19.5%) walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi kutokana na kutoelewa matakwa ya swali, na hivyo kueleza tu migogoro bila kutoa mifano na wengine kutoa majibu yasiyoendana na swali husika. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walitathmini sababu za migogoro ya kisiasa kama vile rushwa, uchu wa madaraka na uchaguzi usio wa haki badala ya kutathmini athari za migogoro katika nchi za Afrika. Kielelezo Na. 1.20 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.

**Kielelezo Na. 1.20**


10 i/ Kunyanganyiwa kwa rasilimali za nchi.
Migogo ilisababishwa kwa kunyanganywa kwa rasilimali za nchi
ii/ Kunyanganywa kwa ardhi yenye rutuba
Migogoro ilisababishwa na kunyanganywa ardhi yenye rutuba.
iii/ kulipishwa kodi
Migogoro ilitokea pale walipoanza kulipa kodi
iv/ Kufanyishwa kazi ujira mdogo.

**Kielelezo Na.1.20:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakukidhi matakwa ya swali na hivyo, kubainisha tu migogoro bila kutoa mifano na hata kutoa majibu yasiyoendana na swali.


## 2.2 SEHEMU B: TAALUMA

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne (4) yaliyogawanywa katika vipengele viwili; kipengele cha Jiografia maswali mawili (2) na kipengele cha Historia maswali mawili (2). Mtahiniwa alitakiwa kuchagua swali moja (1) katika kila kipengele. Kila swali katika sehemu B lilikuwa na jumla ya alama 15. Kufaulu kwa watahiniwa katika sehemu hii kuligawanywa katika makundi matatu kulingana na alama walizopata watahiniwa. Watahiniwa waliopata kati ya alama 0 hadi 5.5 walihesabika kuwa na ufaulu hafifu katika swali husika. Aidha, watahiniwa waliopata alama kati ya 6 hadi 10 walihesabika kuwa na ufaulu wa wastani, na iwapo watahiniwa walipata alama kati ya 10.5 hadi 15 walihesabika kuwa na ufaulu mzuri.

### 2.2.1 Swali 11. Sayari Dunia

Swali la 11 lilitoka katika mada ya Sayari Dunia. Swali hilo lililenga kupima nyanja ya uchambuzi. Mtahiniwa katika swali hili alipaswa kutumia hoja tano kuelezea ushahidi unaodhihirisha kuwa dunia ni duara na sio tambarare.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, jumla ya watahiniwa 1,523 (31.4%) waliofanya mtihani wa Maarifa ya Jamii, walichagua swali hili. Watahiniwa 201 (13.2%) walipata alama kati ya 0 hadi 5.5 ambao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa 1,100 (72.2%) walipata alama kati ya 6 hadi 10 ambao ni ufaulu wa wastani. Watahiniwa 222 (14.6%) walipata alama kati ya 10.5 hadi 15 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla, watahiniwa walifaulu vizuri katika swali hili kwani jumla ya watahiniwa 1,322 (86.8%) walipata alama kati ya 6 hadi 15 ambazo ziliwawezesha kufaulu swali hilo. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na. 11.





**Chati Na. 11**: Inaonesha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 11.


Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa walifanya vizuri katika swali hili kutokana na kuwa na uelewa wa mahitaji ya swali, hivyo kueleza kwa usahihi ushahidi unaodhihirisha kuwa dunia ni duara na sio tambarare. Watahiniwa hao waliweza kueleza hoja mbalimbali zinazothibitisha kuwa dunia ni duara zikiwemo; tukio la kupatwa kwa mwezi, tofauti ya mawio na machweo ya jua kati ya sehemu mbalimbali za dunia, ushahidi wa picha za angani zinazoonesha umbo la dunia na mwonekano wa meli baharini ambapo sehemu ya juu huonekana kwanza kabla ya meli nzima haijaonekana. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri katika swali hili.

**Kielelezo Na. 2.1**


11 Dunia ni sayari ya tatu katika mfumo wa jua ambapo viumbe hai na visivyo kuwa, na uhai kuishi: mfano, binadamu, mimea, wanyama, uchanga.
Ufuatao ni ushahidi unaoonesha kwamba dunia ni duara na siyo tambarare.
Kupatwa kwa mwezi - hii hutokea pale dunia inapokuwa katikati ya dunia jua na mwezi, hivyo kupelekea giza katika mwezi na palendapo huthibitisha kwamba dunia ni duara kwa kuwa kivuli chake ni cha duara;





Kuzama na kuchomoza kwa jua, pia ni ushahidi unaonesha dunia ni duara, watu wa mashariki huona jua likichomoza haraka kuliko wa magharibi hivyo endapo ingekuwa si duara basi wangeona kwa pamoja kuchomoza kwa jua.




11 Muonekano wa meli baharini; pia meli inapokuwa baharini kwa mbali huonekana kama inapanda juu na hivyo kutokuonekana kote, lakini inapokaribia huonekana kama inashuka chini, hivyo dunia ingekuwa si duara, basi ingeonekana kitambo katika eneo tambarare.




Kuzunguka Dunia - Pia wataalamu walifanya uchunguzi wakabaini, endapo utazunguka dunia kuanzia point moja na kuendelea utajikuta umerudi katika point ya kwanza, hivyo endapo dunia ingekuwa si duara huwezi kurudi katika point ya kwanza.




11. Usiku na mchana - Pia wataalam walithibitisha kwamba mzunguko wa dunia unasababisha usiku na mchana, hivyo kwa sababu ni duara pande mbili hupishana katika kupata usiku na mchana hivyo dunia ingekuwa si duara basi pande zote zingepata usiku na mchana kwa pamoja.



Hivyo, kutokana na maelezo hapo juu, ni wazi walimu walikuwa wanafundisha vizuri wanafunzi kuwa dunia ni duara na si tambarare kama wengine wanavyodhani!

**Kielelezo Na. 2.1:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alikuwa na maarifa na ufahamu wa mahitaji ya swali hivyo, kueleza kwa usahihi ushahidi unaodhihirisha kuwa dunia ni duara na sio tambarare.

Hata hivyo, watahiniwa wachache miongoni mwa watahiniwa waliofanya swali hili, walishindwa kujibu swali kwa usahihi kutokana na kutoelewa matakwa ya swali, hivyo kupata alama za chini. Watahiniwa wengine walipata alama chache kutokana na kushindwa kuelezea kwa ufasaha hoja walizozitoa na wengine walitoa ushahidi ambao walishindwa kuuthibitisha kisayansi. Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili vibaya kwani alidhihirisha kwa kutoa hoja kama vile kipenyo cha dunia, usiku na mchana, kushuka na kukua kwa anga na mzingo wa dunia.

**Kielelezo Na. 2.2**

use only

11 Kueleza kwa hoja tano ushahidi unaodhihirisha kwamba dunia ni duara na siyo tambarare.

Dunia ni sayari ambayo ni muhimu katika kuwezesha maisha ya watu kwa upunla na kuwafanya waweze kupata mahitaji yao muhimu.

Ufuatao ni ushahidi unaoelezea au unaodhihirisha kuwa dunia ni duara na siyo tambarare, kama ifuatavyo:-

Kipenyo cha dunia; Katika dunia upo mstari ambao huigawa dunia katika vizio vinnili yaani kizio cha kaskazini na kusini, hivyo mstari huu wa ikweta huta saidia kuthibitisha kama dunia ni duara maana isingekua duara kipenyo kisingekuwepo, maana kitu chenye kipenyo huashiria kama ni duara.

Usiku na mchana; Dunia katika umbo lake la duara upo upande ambao humulikwa na jua na upande mwingine haupati jua, Upande unaopata au unaomulikwa na jua mchana na upande usiopata jua hua usiku, hivyo sababu hii husaidia kuthibitisha kwamba dunia ni duara, na kama isingekua duara ingekua tambarare ingemulikwa na jua yote kusingekua na usiku, siku zote.

Kushuka na kukua kwa anga; Ukitazama angani utagundua kama anga limeshuka kwamba ukiendelea kulifata unaweza kulifikia kitu ambacho naki-

11 hakiwerekani, Umbo hili la dunia pamoj-
a anga lililoshuka hudhihirisha kwamba
dunia ni duara bali sio tambarare.
Mzingo wa dunia; Dunia hujizungu-
sha katika mhimili wake kwa kufuata
mzingo wake, Sababu hutufanya tusiathiri
we na mzunguko huo au tusione mzungu-
ko husika hii ni kwa sababu dunia ni
duara, na kama isingekua duara wakati
dunia inapojizungusha kwenye mhimili
wako binadamu wangeanguka.
Safari za majini; Wakati vyombo vya usafiri
majini Vinapokua mbali baharini tunaanza
kuona Sehemu yake ya juu kabisa mbele
hii humaanisha kwamba dunia ni duara
na ingekua tambarare chombo cha
usafiri majini mfano meli tungeiona yote
inapokua mbali katika bahari.
Hivyo basi; Sayari ya dunia ni duara,
na Sayari hii ni muhimu kwani huweze-
Sha maisha ya binadamu pamoja na kufanya
upatikanaji wa mahitaji muhimu mfano
maji kutoka katika vyanzo vyake.


**Kielelezo Na. 2.2:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakuzingatia matakwa ya swali kwani alitoa ushahidi kuwa dunia ni duara na sio tambarare kwa kutoa hoja kama vile kipenyo cha dunia, usiku na mchana, kushuka na kukua kwa anga na mzingo wa dunia.

### 2.2.2 Swali 12. Nchi Yetu Tanzania

Swali la 12 linatokana na mada ya Nchi Yetu Tanzania. Swali hili lililenga kupima nyanja ya matumizi. Mtahiniwa katika swali hili alitakiwa kueleza faida tano za utalii nchini Tanzania.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, jumla ya watahiniwa 3,321 (68.6%) ya watahiniwa waliofanya mtihani wa Maarifa ya Jamii walichagua swali hili. Watahiniwa 10 (0.3%) walipata alama kati ya 0 hadi 5.5 ambao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa 406 (12.2%)

walipata alama kati ya 6 hadi 10 ambao ni ufaulu wa wastani. Watahiniwa 2,905 (87.5%) walipata alama kati ya 10.5 hadi 15 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla, watahiniwa walifaulu vizuri katika swali hili kwani jumla ya watahiniwa 3,311 (99.7%) walipata alama kati ya 6 hadi 15 ambazo ziliwawezesha kufaulu swali hilo. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na. 12.





**Chati Na. 12**: Inaonesha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 12.

Watahiniwa walifanya vizuri katika swali hili kutokana na kuelewa mahitaji ya swali husika, na hivyo kuwawezesha kueleza shughuli za kiuchumi zinazofanyika nchini Tanzania hususan, faida za utalii nchini. Pia majibu ya watahiniwa yanadhihirisha kuwa, mada ya Nchi Yetu Tanzania ilifundishwa na kueleweka vizuri kwa watahiniwa. Watahiniwa waliojibu swali hilo vizuri, waliweza kueleza faida mbalimbali za utalii nchini Tanzania zikiwemo; kutoa ajira kwa wananchi wa Tanzania, kuingiza fedha za kigeni, kuimarishwa kwa miundombinu sehemu zenye vivutio vya utalii pamoja na utalii kusaidia kuinua sekta nyingine kama vile biashara. Kielelezo Na. 2.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo Na. 2.3**

| | |
|---|---|
| K. | Utalii: Ni kitendo / hali ya mtu kutoka katika eneo lake kwenda eneo lingine kwa lengo la kwenda kutazama vivutio mbali mbali vilivyomo katika eneo hilo. Yawezekana kwa starehe, kujifunza au kujiburudisha. Tanzania ni nchi yenye vivutio vingi vya utalii, ni nchi yenye rasilimali nyingi sana mfano Ziwa Manyara, Mlima Kilimanjaro. Zifuatazo ni faida za utalii nchini Tanzania. |
| | Kukuza uchumi wa nchi Tanzania. Utalii unakuza uchumi wa taifa kutokana na kodi zinazolipwa na watalii wanapoenda katika hifadhi au katika vivutio mbalimbali lakini pamoja la kodi inayolipwa na sekta ya utalii yenyewe. |
| | Chanzo cha ajira: Utalii ni chanzo kimojawapo kinachowapatia watanzania ajira vijana wengi wa kitanzania wamejikita katika sekta ya utalii. Huko wanasimama kama maafisa misitu, watu wanaohusika na kuwatembeza watalii katika hifadhi, madereva wa magari ya hifadhi. |
| | Kusambaza utamaduni wa Kiafrika kwa kupitia utalii. utamaduni wa Afrika unaenea katika maeneo mbalimbali. Wazungu wanapokuja Afrika kutalii huondoka na vitu mbalimbali kutoka Afrika na kuvipeleka kwao wakawapelekea na wenzao kuhusu yale yaliyopo Afrika. |
| | Chanzo cha uwekezaji. Wawekezaji wengi wamewekeza katika sekta ya utalii mfano tunaona mahoteli makubwa yanayojengwa |


12 hao wote ni wawekezaji wanaowekeza. Na kupi
tia uwekezaji huo pato la taifa linainu
lfwa.
Chanzo cha fedha za kigeni: Vile vile
utalii huisaidia nchi yetu kupata fedha
za kigeni. Watalii wanaotoka nchi za
nje huja na fedha wanazozitumia wao
katika nchi zao hivyo kuipatia Tanzania
fedha hizo kama mahpo na kodi.
Kwa kuhitimisha yapo madhara mengi
yatokanayo na utalii ikiwemo kuporomoka
kwa maadili, kuiga maadili kutoka
kwa wazungu.

**Kielelezo Na. 2.3:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alizingatia matakwa ya swali na hivyo kuweza kueleza kwa usahihi shughuli za kiuchumi zinazofanyika nchini Tanzania na faidaza utalii.

Aidha, watahiniwa wachache walipata ufaulu wa wastani kutokana na kushindwa kuelezea kwa ufasaha baadhi ya faida za utalii nchini Tanzania, au kuelezea hoja chache kuliko zilizotakiwa kwenye swali, na watahiniwa wengine kushindwa kutoa maelezo ya kina kutetea hoja walizozitoa. Kielelezo Na. 2.4 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili katika kiwango cha wastani.

**Kielelezo Na. 2.4**

12. Utalii ni kitendo ambacho watu hutoka na kwenda sehemu fulani kwa ajiri ya kuangalia mazingira na hii ni kwa starehe au kujifurahisha, ~~ut~~ utalii upo wa aina mbili ambazo ni Utalii wa ndani na Utalii wa nje. Zipo faida kadha wa kadha za utalii nchini Tanzania zikiwemo;-

Ajira kwa wanaozunguka eneo la chanzo cha utalii;- Kuwaelekeza wageni (watalii) hususani Wazungu baadhi ya sehemu, hujipatia ajira

Fedha za kigeni;- mfano;- watalii wa nje;- huwa wanapoingia nchini kutalii huja na pesa au fedha za kigeni na hivyo kupelekea nchi kupata fedha za kigeni.

Kukuza au kuongeza pato la nchi; mfano;- watalii wa ndani na nje pia; huwa hulipia kiasi fulani cha fedha pale wanapoenda kutembelea vivutio vya utalii

Kukuza ushirikiano wa kimataifa;- Wageni wapofika toka nchi za kigeni na kuondoka salama watafurahia uwijanja nchi kuongeza marafiki

Kuongezeka kwa wawekezaji;- Baada ya watalii kutembelea nchi yetu hukutana na malighafi nyingi na wengine hushawishika kuja kuwekeza nchini Tanzania


Utalii ni muhimu sana kwa Tanzania serikali iongeze ulinzi na usalama kwa watalii.

**Kielelezo Na. 2.4:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakuzingatia matakwa ya swali kwani hakuweza kuelezea kwa ufasaha baadhi ya faida za utalii nchini Tanzania.

### 2.2.3 Swali 13. Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika

Swali la 13 lilitoka katika mada ya Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika hususan, katika mada ndogo ya Asili na Mabadiliko ya Binadamu, Teknolojia na Mazingira. Swali hili lililenga kupima nyanja ya uchambuzi ambapo, mtahiniwa alitakiwa kutambua uhusiano uliopo kati ya mabadiliko ya kiteknolojia na mabadiliko ya mifumo ya uzalishaji mali. Mtahiniwa alipaswa kuonesha namna ambavyo mfumo wa maisha ya Ujima unatofautiana na mfumo wa maisha ya kibepari.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, jumla ya watahiniwa 423 (8.7%) ya watahiniwa waliofanya mtihani wa Maarifa ya Jamii, walichagua swali hili. Watahiniwa 64 (15.1%) walipata alama kati ya 0 hadi 5.5 ambao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa 143 (33.8%) walipata alama kati ya 6 hadi 10 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 216 (51.1%) walipata alama kati ya 10.5 hadi 15 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla, watahiniwa walifaulu vizuri katika swali hili kwani jumla ya watahiniwa 359 (84.7%) walipata alama kati ya 6 hadi 15 ambazo ziliwawezesha kufaulu swali hilo. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na. 13.




**Chati Na. 13**: Inaonesha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 13.

Watahiniwa walijibu swali hili kwa usahihi kwa sababu walielewa matakwa ya swali. Ingawa swali hili lilitoka nje ya muhtasari wa Ualimu Daraja A, watahiniwa walihawilisha maarifa waliyojifunza Elimu ya Sekondari na katika mada ya Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika na Zanzibar na Kwingineko Afrika hususan, katika mada ndogo ya Asili na Mabadiliko ya

Binadamu, Teknolojia na Mazingira. Kielelezo Na. 2.5 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua vizuri swali hili.

**Kielelezo Na. 2.5**

13. Katika maendeleo ya maisha ya binadamu, tumepitia mifumo minne ya maisha ambayo ni Ujima, Ukabaila, Ubepari na Ujamaa. Ujima ni mfumo wa maisha wa kwanza ambapo watu waliishi kwa pamoja na kushirikiana katika masuala yote. Ubepari ni mfumo wa maisha ambao kundi fulani la watu wenye uwezo wanashikilia uchumi na masuala yote katika jamii. Ufuatao ni utofauti kati ya mfumo wa maisha wa Ujima na Ubepari:-

Katika mfumo wa Ujima mali zote zilikuwa zikimilikiwa na jamii nzima, mfano mashamba na mifugo yalikuwa chini ya uangalizi wa jamii nzima, wakati katika mfumo wa Ujima mali zote za thamani zilikuwa zikimilikiwa na watu wachache wenye uwezo tu. Mashamba mifugo na mali nyingine zilikuwa zikimilikiwa na watu wachache wenye utajiri katika jamii.


Katika mfumo wa Ujima hapakuwa na unyonyaji wa aina yoyote kwani mambo yote yalifanyika kwa usawa, kila mwanajamii alipata haki sawa na wenzake. Wakati katika mfumo wa Kibepari palikuwepo na unyonyaji wa hali ya juu. Watu wenye uwezo waliwanyonya watu wenye

13 uchumi mdogo kwani walimiliki ardhi kubwa na yenye rutuba kwa ajili ya kuzalisha mazao mbalimbali na shughuli nyingine kama ufugaji. Pia watu wali kuwa wakifanya kazi kubwa na kulipwa ujira mdogo sana.

Katika mfumo wa Ujima hapakuwa na matabaka miongoni mwa wanajamii. Hapakuwa na matabaka ya wenye nacho na wasiokuwa nacho wote waliishi kwa usawa. Wakati katika mfumo wa Kibepari palikuwepo na matabaka kati ya wenye nacho na wasiokuwa nacho. Wanajamii wenye kipato cha chini hawakuweza kuendana na watu wenye uwezo/kipato kikubwa.

Katika mfumo wa Ujima hapakuwa na Ubaguzi wa Kijinsia bali palikuwa na mgawanyo sahihi wa kazi kwa watoto wa kiume na wakike. Wakati mfumo wa Kibepari Ubaguzi wa kijinsia ulikuwepo na hapakuwa na mgawanyo sahihi wa kazi kwa wanaume na wanawake. Wanawake hawakushirikishwa katika kumiliki mali.

Katika mfumo wa ujima watu waliishi kwa misingi ya kuheshimiana na kupendana ambapo walidumisha amani na upendo miong oni mwa wanajamii wakati katika


13 mfumo wa Kibepari watu hawakuishi kwa upendo na migogoro mingi miepka baina ya watu katika jamii.
Kwa ujumla kuna tofauti iliyopo baina ya mfumo wa Ujima na Kibepari. Katika mfumo wa Kibepari tumeona kwamba watu wenye kipato cha chini wamekuwa wakikandamizwa kwa namna mbalimbali kwani pia walikuwa wakitozwa kodi nyingi ambapo iliwalazimu wafanye kazi ngumu kwa wenye uwezo na kupata fedha kidogo.

**Kielelezo Na. 2.5:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyezingatia matakwa ya swali na kuweza kuhawilisha maarifa.

Aidha, baadhi ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za chini. Sababu za kushindwa kujibu vizuri swali hili ni kutokana na kutofuata maelekezo ya swali. Mfano, baadhi ya watahiniwa walielezea zaidi maisha ya mfumo wa ujima bila kuonyesha tofauti iliyopo na mfumo wa kibepari. Kielelezo 2.6 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.


**Kielelezo Na. 2.6**

13. Ujima ni mfumo ambao binada-
mu aliishi kwa kuthaminiana na kuwa
kama ndugu ilihali mfumo wa ubepari
ni mfumo ambao ulikuwa wa mabavu na
watu walitumikishwa na kufanywa watu-
mwa katika ardhi yao wenyewe bila
kupinga.

Tofauti iliyopo katika mfumo wa
Ujima na ule mfumo wa kibepari
katika maisha.

Haukuwa na unyonyaji katika mfumo
wa ujima binadamu hakunyonywa kwa
lolote lile katika maisha yake aliyo
ishi. Watu waliishi na kuondoa woga wa
kunyonywa na mabepari walivamia taifa
la Afrika.

Walifanya kazi kwa pamoja binada-
mu wakati wa uzalishaji mali katika


13. kipindi cha ~~map~~ mabepari, walitengana na ku-
fanya kazi ambayo haikuwa na uthamani
kwao ili hali ilikuwa inawafaidisha mabe-
beru waliokuwa wakiwatumikisha katika ardhi
yao.
Haukuwa na watumwa, mfumo wa ujima
uliweza kuwanufaisha watu kwa kila
mmoja kufanya kitu ambacho kilikuwa
na manufaa kwa wao wenyewe sio
kwa mtu mwingine ambaye hakuweza
kujishughulisha.
Walizalisha mali kwa pamoja, waka-
ti wa mfumo wa ujima muda wa kwe-
nda kuzalisha mali shambani, wazee wa-
toto na wagonjwa ..ambao waliweza kuba-
ki nyumbani na kuhudumiwa kwa kuth-
aminiwa.
Haukuwa na unyanyasaji katika mfumo
wa maisha ya ujima, watu, wa'li ~~[illegible]~~ kuwe-
za kunyanyasana labda kwa sie ni mzee
mtoto au mlemavu. Walijichukulia kama
ndugu na kupendana bila kuwa na
unyanyasaji wala ubaguzi wa aina yoyote
ile.
Mfumo huu wa ujima ni mfumo
ambao uliendana na mfumo wa ujamaa
ambapo binadamu alitumia akili katika
uzalishaji wake na hatimaye kuweza ku-
faidika katika jamii nzima bila kuwa
na migogoro yoyote katika uzalishaji au
umiliki wa mali.


**Kielelezo Na. 2.6:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakufuata maelekezo ya swali kwa kuelezea zaidi maisha ya mfumo wa Ujima bila kuonyesha tofauti iliyopo na mfumo wa kibepari.

### 2.2.4 Swali 14. Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika

Swali limetokana na mada ya Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika. Swali hilo lililenga kupima uundaji. Mtahiniwa alitakiwa kutumia mifano

kuainisha shughuli kuu tano za kiuchumi zilizofanyika wakati wa uchumi wa kikoloni barani Afrika.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, jumla ya watahiniwa 4,420 (91.2%) ya watahiniwa waliofanya mtihani wa Maarifa ya Jamii, walichagua swali hili. Watahiniwa 169 (3.8%) walipata alama kati ya 0 hadi 5.5 ambao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa 2,270 (51.4%) walipata alama kati ya 6 hadi 10 ambao ni ufaulu wa wastani. Watahiniwa 1,981 (44.8%) walipata alama kati ya 10.5 hadi 15 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla, watahiniwa walifaulu vizuri katika swali hili kwani jumla ya watahiniwa 4,251 (96.1%) walipata alama kati ya 6 hadi 15 ambazo ziliwawezesha kufaulu swali hilo. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na. 14.




**Chati Na. 14**: Inaonesha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 14.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa walifanya vizuri katika swali hili kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha wa matakwa ya swali. Kwa mfano, waliweza kuelezea baadhi ya shughuli zilizofanyika wakati wa ukoloni kama vile; kilimo cha mashamba makubwa, uchimbaji madini, biashara, usafirishaji na uchukuzi. Hii inadhihirsha pia kwamba, mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji katika mada hii ulifanikiwa. Kielelezo Na. 2.7 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo Na. 2.7**

14. SHUGHULI KUMI TANO ZA KIUCHUMI ZILIZOFANYIKA WAKATI WA UCHUMI WA KIKOLONI BARANI AFRIKA

Uchumi wa kikoloni barani afrika; hizi ni shughuli za uzalishaji mali zilizokuwa zikifanywa na wakoloni wakati wa utawala wao barani afrika. shughuli hizi za kiuchumi zililenga kuwapatia malighafi ambazo zingetumika katika kuzalisha bidhaa katika viwanda vyao huko ubaya. ~~[illegible]~~ shughuli za kiuchumi zilifanywa na waafrika huku wakiwa katika usimamizi. mkali wa wazungu au wakoloni.

Zifuatazo ni shughuli za kiuchumi zilizofanywa wakati wa uchumi wa kikoloni barani afrika

Shughuli ya kilimo; hii ndiyo shughuli kuu iliyofanywa na wakoloni barani afrika ambapo walilenga kuzalisha malighafi ambazo zingetumika kutengeneza bidhaa mfano wa malighafi hizo zilikuwa ni katani ambapo ililimwa tanga, pamba, kahawa ambayo ililimwa bukoba, kilimanjaro, maeneo ambayo yalikuwa yanafaa kwa kilimo ni yale yenye rutuba tu huyo mazao yaliyolimwa

14 ni mazao ya biashara kama kahawa, chai, katani, pamba, karafuu ili kupeleka ulaya kusalisha au kutengeneza bidhaa na watu walilazimishwa kufanya kazi katika mashamba ya walowezi.

Shughuli ya uchimbaji wa madini, hii ni shughuli nyingine iliyofanywa watawala wa ukoloni barani afrika ambapo shughuli hii ilifanyika nchini afrika kusini, zimbambwe, tanganyika ambapo wananchi wenye nguvu walichukuliwa kwa nguvu kama manamba na kwenda kufanya kazi ya kuchimba madini, vilevile watu walinyang'anywa pasi za kusafiria, shughuli hii ilelenga kupata madini ambayo yangetumika kutengeneza vitu mbalimbali vya thamani ambapo walichimba na uchimbaji wa dhahabu kutoka afrika kusini na zimbabwe, madini ya shaba, madini ya chuma,

Shughuli ya biashara; Hii ni shughuli nyingine iliyofanywa watawala wa ukoloni barani afrika ambapo baada ya malighafi kusafirishwa afrika na kupelekwa ulaya, wakoloni walirudisha nguo ambazo zimetengenezwa na kuwauzia waafrika kwa bei ya juu au kwa kubadilishana na vitu vya thamani ambapo bidhaa zilizouzwa ni kama vile hereni, shanga, nguo, mitutu na waafrika walitoa madini, pembe za ndovu, ngozi za wanyama, hivyo shughuli hii pia ilifanywa na wazungu walipata sana faida kutokana na shughuli ya biashara.

Shughuli ya viwanda; Hii ni shughuli nyingine iliyofanywa na watawala wakati wa utawala wao barani afrika ambapo viwanda vilivyotengenezwa ni vile vya kuondoa uzito wa malighafi na

14 kuzifanya kwa nyepesi, mfano kiwanda cha kubangua korosho, kiwanda cha kuchakata mkonge kilichojengwa tanga na kiwanda cha kuchakata pamba ambapo viwanda hivi vilitumwa na lengo la kuondoa uzito wa malighafi.


Shughuli ya usafirishaji na uchukuzi; hii ni shughuli mojawapo pia ambayo ilifanywa wakati wa uchumi wa kikoloni ambapo barabara mbalimbali zilianzishwa ili kuwezesha usafirishaji wa malighafi kutoka afrika kwenda ulaya, vilevile barabara na reli zilianzishwa mfano reli ya tazara ili kuwezesha kusafirisha malighafi kutoka mashambani na kuweza kuzipeleka ulaya kwenye viwanda vyao. hivyo shughuli ya usafirishaji pia ni mojawapo ya shughuli zilizofanywa wakati wa uchumi wa kikoloni barani afrika.

Hivyo basi; uchumi wa kikoloni ulitumwa na lengo la kuinyonya nchi za kiafrika na kuweza kutunasha mataifa ~~ma~~ yao ambapo hadi sasa hivi ~~makoloni~~ ya nchi za ulaya zinaendelea kutunyonya waafrika bila siri kupitia mfano katika sekta ya madini. hivyo ni bora waafrika wasomi na waweze kujikomboa na ukoloni huu mamboleo ambao mpaka sasa hivi unaendelea barani afrika.

**Kielelezo Na. 2.8**: Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alizingatia matakwa ya swali na hivyo, kuainisha shughuli zilizofanyika wakati wa uchumi wa kikoloni barani Afrika kwa usahihi na kwa mtiririko mzuri.

Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa walishindwa kujibu swali vizuri kutokana na kuainisha shughuli chache zenye maelezo yasiyokidhi matakwa ya swali ambalo lilimtaka aanishe shughuli kuu tano zilizofanyika wakati wa uchumi wa kikoloni barani Afrika. Kielelezo Na. 2.8 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili.

**Kielelezo Na. 2.8**



14. Ukoloni ni hali ya nchi au
Taifa lenye nguvu kuingoza taifa au
kulitawala taifa dhaifu kiuchumi, siasa,
utamaduni, Uchumi wa kikoloni ni yale
mambo yote ambayo wakoloni walifanya
ili kujinufaisha wenyewe na nchi zao.
Zifuatazo ni shughuli kuu za
kiuchumi zilizofanyika wakati wa uchumi
wa kikoloni Barani Afrika
Kutafuta malighafi, wakoloni
walifanya kilimo cha mashamba makubwa
na madogo ili kupata malighafi ambazo
zilitumika katika viwanda vyao.
Vibarua wa bei rahisi, Walihitaji
vibarua hao wa bei rahisi ili wakauzwe
katika soko la watumwa na kupatiwa
fedha serikali ya kikoloni.
Kuongezwa kwa kodi, Zilongezwa
kodi mfano kodi ya kichwa, kodi ya
matiti ambazo zilikusanywa na wakoloni
na kuzipeleka katika serikali yao
na hivyo kusababisha kuongezeka kwa
uchumi wa wakoloni.
Biashara ya kubadilishana bidhaa
kwa bidhaa ili kupeleka wakoloni kuwa.
badilishwa waafrika kutu vyao mfano
Ndio na kubadilishana na madini
ya thamani sana.
Hivyo basi, Wakoloni walifanya
shughuli mbalimbali katika Bara la Afrika
kwa ajili ya manufaa ya nchi zao
na mataifa yao.

**Kielelezo Na. 2.8**: Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alitoa maelezo yasiyokidhi matakwa ya swali kwa kuainisha shughuli chache tu zilizofanyika wakati wa uchumi wa kikoloni barani Afrika badala ya shughuli kuu tano zilizotakiwa katika swali husika.


## 2.3 SEHEMU C: UFUNDISHAJI

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili ya ufundishaji kutoka katika masomo ya Jiografia na Historia. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu hii, ambapo kila swali lilikuwa na alama 15. Kufaulu kwa watahiniwa katika sehemu hii kuligawanywa katika makundi matatu kulingana na alama walizopata watahiniwa. Watahiniwa waliopata kati ya alama 0 hadi 5.5 walihesabika kuwa na ufaulu hafifu katika swali husika. Aidha, watahiniwa waliopata alama kati ya 6 hadi 10 walihesabika kuwa na ufaulu wa wastani, na iwapo watahiniwa walipata alama kati ya 10.5 hadi 15 walihesabika kuwa na ufaulu mzuri.

### 2.3.1 Swali 15. Maandalizi ya Kufundisha na Kujifunza

Swali la 15 lilitoka katika mada ya Maandalizi ya Kufundisha na Kujifunza. Swali hili lililenga kupima nyanja ya matumizi, ambapo mtahiniwa alitakiwa kueleza umuhimu wa muhtasari wa somo la Jiografia katika ufundishaji na ujifunzaji.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walichagua swali hili. Watahiniwa 21 (0.4%) walipata alama kati ya 0 hadi 5.5 ambao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa 873 (18%) walipata alama kati ya 6 hadi 10 ambao ni ufaulu wa wastani. Watahiniwa 3,950 (81.6%) walipata alama kati ya 10.5 hadi 15 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla, watahiniwa walifaulu vizuri katika swali hili kwani jumla ya watahiniwa 4,823 (99.6%) walipata alama kati ya 6 hadi 15 ambazo ziliwawezesha kufaulu swali hilo. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na. 1.




**Chati Na. 15**: Inaonesha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 15.

Watahiniwa walifanya vizuri katika swali hili kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha na kuzingatia matakwa ya swali. Aidha, ilikuwa rahisi kukumbuka umuhimu wa muhtasari katika ufundishaji kwa kuwa, ni mojawapo ya vifaa muhimu vya mtaala ambavyo mtahiniwa alivitumia wakati wa mazoezi ya kufundisha kwa vitendo (BTP). Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri katika swali hili.

**Kielelezo Na. 3.1**

15. Muhtasari ni mpango kazi unaotumiwa na mwalimu kuandaa Azimio la kazi kwa kuangalia mada kutoka kati ka muhtasari wa somo ambao kujumuisha mada zote zinazo takiwa kufundishwa kwa darasa husika kwa kipindi chote kwa kuzingatia mpangilio mzuri kama ilivyo katika muhtasari mfano muhtasari kuonyesha idadi ya mada pamoja na vipindi na zana zinazo takiwa kutumika katika ufundishaji na ujifunzaji Umuhimu wa muhtasari wa somo la Jiografia katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji:

Muhtasari kwa mwalimu wa somo la jiografia kumsaidia mwalimu kuandaa mpango kazi wake unaweza kuwa kwa muhula au mwaka mzima mwalimu kutumia muhtasari kuandaa Azimio lake la kazi kwa kuzingatia idadi ya vipindi pamoja na idadi ya vipindi mwalimu kuzingatia idadi ya mada.


Mwalimu kutumia muhtasari kama mwongozo kwa kuangalia shughuli za kutendwa na mwalimu na kutofautisha na shughuli za kutendwa na mwanafunzi kwa kupata mwongozo kutoka katika muhtasari wa somo jambo ambalo kuongeza ubora wa ufundishaji kwa mwalimu kufundisha kwa kufuata mwongozo kama ilivyo katika muhtasari wa somo la jiografia.

15. muhtasari kumsaidia mwalimu kuchagua na kuandaa<br>mbinu na zana bora za kufundishia na kujifunzi kwa<br>kuangalia mada pamoja namna ya kutumia mbinu mbalimbali<br>kwa mwalimu kupata mwongozo ni zana gani kutumika kufu<br>ndishia mada husika darasani.<br>Mwalimu kutumia muhtasari ni vigumu kwenda<br>nje ya somo kwa kufundisha tofauti na malengo ya somo<br>ni rahisi kwa mwalimu kufuata taratibu zote kwa kuang<br>alia muhtasari kumwongoza kufanya nini mfano mwalimu<br>kufuata mpangilio wa mada kwa kuangalia uhusiano kati ya<br>mada moja na mada nyingine.<br>Muhtasari kumsaidia mwalimu kutambua mambo<br>muhimu ya kuzingatia pia mwalimu kutumia mhtasari wa<br>somo la jiografia kuchagua mada za kufanyia upimaji mfan<br>o katika kutunga zoezi, jaribio au mtihani mwalimu kuangali<br>a mada zote zilizomo katika muhtasari na kutunga maswali<br>kulingana na muhtasari wa somo la jiografia.<br>Hivyo basi ni kweli kwamba ufanisi katika ufundi<br>shaji na ujifunzaji wa somo la jiografia hutegemea uwepo<br>wa muhtasari wa somo kwa kuangalia umuhimu wa<br>muhtasari wa somo kwa mwalimu kwa kuonekana kama<br>nahodha wa meli majini kwa kuwa ndio mwongozo.

**Kielelezo Na. 3.1**: Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyekuwa na maarifa ya kutosha kuhusiana na muhtasari.

Licha ya watahiniwa wengi (96.2%) kujibu swali hili kwa usahihi, watahiniwa wachache (3.8%) walishindwa kujibu vizuri. Sababu ya kushindwa kujibu swali hili ni kukosa maarifa na maelezo ya kutosha kuhusu umuhimu wa muhtasari wa somo la Jiografia katika ufundishaji na ujifunzaji. Kielelezo 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya katika swali hili ambapo alitoa tu utangulizi na hakuendelea kufafanua hoja.

**Kielelezo Na. 3.2**





**Kielelezo Na. 3.2:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakuwa na maarifa na maelezo ya kutosha kuhusu umuhimu wa muhtasari na hivyo, kutoa utangulizi tu bila ya hoja yoyote.

### 2.3.2 Swali 16. Uchambuzi wa Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali la 16 lilitoka katika mada ya Uchambuzi wa Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia somo la Historia na lililenga kupima nyanja ya matumizi. Katika swali hili, mtahiniwa alipaswa kueleza kwa kina umuhimu wa mwalimu wa somo la Historia kutumia zana za kufundishia na kujifunzia wakati wa tendo la ufundishaji na ujifunzaji.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walijibu swali hili. Watahiniwa 68 (1.4%) walipata alama kati ya 0 hadi 5.5 ambao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa 1,792 (37.1%) walipata alama kati ya 6 hadi 10 ambao ni ufaulu wa wastani. Watahiniwa 2,980 (61.5%) walipata alama kati ya 10.5 hadi 15 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla, watahiniwa walifaulu vizuri katika swali hili kwani jumla ya watahiniwa 4,772 (98.6%) walipata alama kati ya 6 hadi 15 ambazo ziliwawezesha kufaulu swali hilo. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na. 16.




**Chati Na. 16**: Inaonesha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 16.

Watahiniwa waliweza kujibu swali hili kwa usahihi kwa sababu walizingatia matakwa ya swali husika. Aidha, baadhi ya watahiniwa walieleza vizuri hoja zao na kuzipanga katika mtiririko unaotakiwa kuanzia utangulizi, kiini hadi hitimisho. Kielelezo Na. 3.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili.

**Kielelezo Na. 3.3**

16. Zana ni vifaa ambavyo huweza kutumika ili kurahisisha shughuli fulani. Zana za kufundishia na kujifunzia ni vifaa ambavyo huandaliwa na mwalimu kwa ajili ya kutumika wakati wa kipindi ili kurahisisha kufikiwa kwa lengo lililokusudiwa. Zana hizo zinaweza kupatikana kupitia njia tofauti ikiwemo kununua, kuomba, kutengeneza, kufaragua na kukusanya.


Mwalimu wa somo la Historia anapaswa kutumia zana za kufundishia na kujifunzia katika ufundishaji wake kwa zina umuhimu kwa wanafunzi kama ifuatavyo:-

Kuchochea udadisi. Zana bora na nzuri yenye kuvutia husaidia kumfanya mwanafunzi awe mdadisi kutaka kujua ukweli wa jambo fulani. Matumizi bora ya zana humwezesha mwanafunzi kuwa mdadisi katika mambo anayojifunza kwa undani zaidi.

Kurahisisha somo. Matumizi mazuri ya zana husaidia kuondoa utata na ugumu wa maudhui hivyo kuwafanya watoto kuelewa kwa urahisi kile kilichokusudiwa kufundishwa na mwalimu wakati wa kipindi chake.

Kujenga kumbukumbu ya kudumu. Kujifunza kwa kushirikisha viungo mbalimbali vya mwili na milango ya fahamu inasaidia kutunza kwa muda mrefu kile kilichofundishwa mfano. Ni rahisi kwa mwanafunzi aliyeona na kushiriki kukumbuka kuliko yule anahadithiwa kwa nadharia.

Kuleta ushirikiano. Matumizi ya zana huweza kuibua ushiriki mzuri wa wanafunzi



16 darasani wakati wa kipindi. Hii kuwawezesha
wanafunzi kudumisha ushirikiano na urafiki
baina yao pia kuweza kumpenda mwalimu
wao kupitia mazungumzo na mawasiliano
mema yaliyopo katika mchakato mzima wa ujifunzaji
Husaidia kuleta ari ya kujifunza. Kupitia
mwanafunzi kujifunza hasa kwa vitendo inamsa-
idia kuelewa somo na kuweza kulipenda
katika kujifunza. Hii humwezesha pia mwali-
mu kutumia maelezo na nguvu kidogo katika
ufundishaji wake kuliko yule anayefundisha
kuku wanafunzi wake wamechukia somo lake.
Hivyo basi. Japo kuwa kuna umuhimu
sana wa mwalimu wa somo la Historia kutumia
zana pia ni muhimu kuwa na uwezo wa kuzitu-
mia kwa kuzingatia matumizi bora na tahadhari
kwani baadhi ya zana huweza kusababisha
ajali, kuwa chanzo cha kelele pia kuzalilisha.

**Kielelezo Na. 3.3**: Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alikidhi matakwa ya swali hivyo, kutoa hoja sahihi na kuzipanga katika mtiririko unaotakiwa kuanzia utangulizi, kiini hadi hitimisho.

Baadhi ya watahiniwa wachache (1.4%) walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi kwani walishindwa kutoa hoja sahihi kuhusu umuhimu wa mwalimu kutumia zana wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la historia. Baadhi ya watahiniwa walichanganya hoja za umuhimu wa zana kwa mwanafunzi na umuhimu wa somo la historia kwa mwanafunzi. Kielelezo Na. 3.4 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili kwa kuelezea umuhimu wa somo la Historia badala ya kuelezea umuhimu wa mwalimu kutumia zana wakati ufundishaji na ujifunzaji.

**Kielelezo Na. 3.4**

16. Historia maana yake ni
kujua mambo yaliyopita zamani,
yaliyopo na mambo yajayo, hivyo
ukifundisha historia ili kutunza kumbu
kumbu za vitu, mwalimu anapo
fundisha somo la historia anapaswa
kuwa sana pale anapo kumm
mfano mbalimbali ya zana za kale.
Umuhimu wake mwalimu
wa somo la historia ni kama
ufuatavyo:
Kuwajengea wanafunzi
kujua historia ya nchi kupitia
historia ya mwalimu wanafunzi
kutambua na kujua lini na
wapi nchi yetu ilipata uhuru na
kujikomboa kutoka kwa mabeberu.
Kuwajengea wanafunzi
kujua historia ya binadamu
mfano wanafunzi wameweza
wakiuliza binadamu alitoka wapi
sasa kwa kutumia mifano ya chimpanzi tunajua
Kuwajengea wanafunzi
kutambua zana za kale



16 Kuwafanya wanafunzi
Kutambua chimbuko la mtu,
mabadiliko binadamu enzi ya kale
jinsi mtu alivyokua wapi kupitia
kupitia mwalimu na mifano yake
ya uhimbi na uhimbombo wanafunzi wajue
Kuwafanya wanafunzi
waelewe historia kabla na baada
ya uhuru, kwa umuhimu wa
mwalimu wa somo la histo
ria ambapo ambapo mwalimu
atatumia mifano ya wakoloni
walio tutawala mifano wajerumani
mari; waingereza.
Kulingana na maelezo
hayo kwa ndio umuhimu wa mwa
limu wa somo la historia
ambapo tunapaswa kujifunza hiyo
na kuyafahamu.

**Kielelezo Na. 3.4:** Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakuzingatia matakwa ya swali kwani alichanganya hoja za umuhimu wa zana kwa mwanafunzi na umuhimu wa somo la historia kwa wanafunzi.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA

Mtihani somo la Maarifa ya Jamii ulikuwa na maswali kumi na sita (16) yaliyotoka katika mada kumi (10) za masomo ya Jiografia na Historia. Kati ya mada hizo, mada tano (5) ni za somo la Jiografia na mada tano (5) ni za somo la Historia.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika mada mbalimbali unaonesha kuwa, watahiniwa walikuwa na kiwango kizuri sana cha ufaulu katika mada zote kwa wastani wa asilimia 90.3. Mada hizo ni: Sayari Dunia (92.8%); Nchi Yetu Tanzania (95.4%); Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani (90.8%); Uchambuzi wa Zana za Kufundishia na Kujifunzia somo la Jiografia (99.6%); Uchambuzi wa Vifaa na Zana za Kufundishia na

Kujifunzia somo la Historia (98.6%); Mifumo ya Uzalishaji na Maendeleo ya Binadamu (84.9%); Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika (82.9%); Mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi katika Afrika huru (86.7%); Ushirikiano wa Kimataifa (95.4%) na mada ya Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika, ambayo kiwango chake cha ufaulu kilipungua kidogo (75.0%) ikilinganishwa na mada nyingine.

Kwa ujumla, watahiniwa wameweza kufaulu katika mada mbalimbali kwa sababu walikuwa na umahiri wa kutosha katika mada husika. Kiwango hiki kizuri cha ufaulu kinadhihirisha kuwa, wakufunzi walikamilisha mada zao kwa kuwapa watahiniwa maarifa na weledi wa kutosha na hivyo, kuwaandaa vema kwa ajili ya mtihani wa Maarifa ya Jamii. Muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa kwa mada umeoneshwa katika Jedwali Na. 3.1.

**Jedwali Na. 3.1: Muhtasari waUfaulu wa Watahiniwa kwa Mada**

| Na. | Mada | Idadi Ya Maswali | % ya Watahiniwa Waliopata Alama za Wastani au Zaidi | Wastani wa Ufaulu kwa Mada | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Uchambuzi wa Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Jiografia | 15 | 99.6 | 99.6 | Mzuri |
| 2. | Uchambuzi wa Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Hisitoria | 16 | 98.6 | 98.6 | Mzuri |
| 3. | Nchi Yetu Tanzania | 2 | 73.8 | 95.4 | Mzuri |
| | | 4 | 99.0 | | |
| | | 12 | 99.7 | | |
| 4. | Ushirikiano wa Kimataifa | 9 | 95.4 | 95.4 | Mzuri |
| 5. | Sayari Dunia | 1 | 98.7 | 92.8 | Mzuri |
| | | 11 | 86.8 | | |
| 6. | Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani | 3 | 85.2 | 90,8 | Mzuri |
| | | 5 | 96.3 | | |
| 7. | Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi katika Afrika Huru | 8 | 81.9 | 86.7 | Mzuri |
| | | 10 | 91.4 | | |
| 8. | Mifumo ya Uzalishaji na Maendeleo ya Binadamu | 13 | 84.9 | 84.9 | Mzuri |
| 9. | Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika | 6 | 82.9 | 82.9 | Mzuri |
| 10. | Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika | 7 | 63.3 | 75.0 | Mzuri |
| | | 14 | 86.8 | | |

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, upimaji wa Ualimu Daraja A katika somo la Maarifa ya Jamii mwaka 2018 ulizingatia mihutasari wa masomo wa ya Jiografia na HIstoria ya mwaka 2009. Maswali yote pia yalizingatia ngazi zote za majazi ya utambuzi zikiwemo; nyanja ya maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini. Kiwango cha kufaulu kwa watahini katika mtihani huo kilikuwa kizuri na cha kuridhisha ambapo wastani wa kufaulu ulikuwa ni asilimia 90.3.

Uchambuzi huu unabainisha changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kutafutiwa ufumbuzi kwa lengo la kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza na hivyo, kuboresha kiwango cha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Maarifa ya Jamii. Changamoto hizo ni kama; watahiniwa wachache kukosa uelewa wa maswali, kushindwa kutoa majibu sahihi kulingana na matakwa ya swali. Pia, baadhi ya watahiniwa kukosa umakini na hivyo, kujikuta wakichanganya hoja ambazo hazihusiani kabisa na swali husika. Ili kuboresha kiwango cha ufaulu kwa wanachuo wa Ualimu wa Daraja A katika mtihani wa Maarifa ya Jamii, mkazo zaidi unahitajika katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada zote kwa kutumia njia shirikishi ili kuwajengea wanachuo umahiri wa kutosha katika mada zote zilizoanishwa katika mihutasari.

Taarifa hii ya upimaji itasaidia kutoa mrejesho kuhusu namna mada za somo la Maarifa ya Jamii zilivyofundishwa vyuoni na hivyo, kuonesha maeneo yenye upungufu katika ufundishaji na ujifunzaji ili kutoa fursa nzuri zaidi kwa wakufunzi, wanachuo na wakuza mitaala kuboresha mitaala na ufundishaji na ujifunzaji kwa mada ambazo watahiniwa hawakufanya vizuri na hivyo, kuboresha ufaulu wa watahiniwa kwa miaka ijayo.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu katika mtihani wa Maarifa ya Jamii inapendekezwa kuwa:-

(i) Wakati wa ufundishaji na ujifunzaji, wakufunzi waweke mkazo katika mada zote za Taaluma na Ufundishaji kwenye masomo ya Historia na Jiografia ili kuleta uwiano mzuri wa ufaulu katika mada kwenye masomo husika.

(ii) Wakufunzi waweke mkazo pia katika matumizi ya mbinu shirikishi hususan, mbinu ya majadiliano na kazi mradi katika mada ya Utawala

na Uchumi wa Kikoloni Afrika ambayo imeonekana kuwa na kiwango cha chini cha kufaulu ikilinganishwa na mada nyingine ili kuwajengea wanachuo uwezo mkubwa wa kuwasilisha hoja zao kwa kuongea na kimaandishi, na hivyo kuwasaidia kujibu vizuri maswali ya insha katika mtiririko unaotakiwa wawapo vyuoni na hatimaye, katika mtihani wa Taifa.

(iii) Aidha, watahiniwa wengi wamebainika kupata ufaulu hafifu kwenye baadhi ya maswali kutokana na kutokuwa makini wakati wa kusoma maswali na hivyo kujibu maswali kinyume na matakwa ya maswali hayo. Hivyo, inashauriwa kuwa, wakufunzi wasisitize umuhimu wa watahiniwa kusoma kwa makini maswali kabla ya kuyajibu ili wajenge mazoea ya kujibu maswali kulingana na walichoulizwa. Hii itasaidia watahiniwa wengi kutoa majibu yanaoyoendana na maswali waliyoulizwa ili kuepuka kuchanganya dhana wakati wa kujibu maswali hayo.

# KIAMBATISHO

**Jedwali Na. 5.1:** Vigezo vya ufaulu vilivyotumika katika uchambuzi wa  kila swali.

| **Sehemu** | **Namba ya swali** | **Alama stahiki katika swali** | **Alama walizopata watahiniwa** | **Kiwango cha ufaulu** |
|---|---|---|---|---|
| A | 1-10 | 4 | 3-4 | Vizuri |
| | | | 2-2.5 | Wastani |
| | | | 0-1.5 | Hafifu |
| B | 11-14 | 15 | 10.5-15 | Vizuri |
| | | | 6-10 | Wastani |
| | | | 0-5.5 | Hafifu |
| C | 15-16 | 15 | 10.5-15 | Vizuri |
| | | | 6-10 | Wastani |
| | | | 0-5.5 | Hafifu |

cmyk